

HALI YA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI MISRI HISTORIA NA MAENDELEO

ALAA SALAH

This article discusses the uses and teaching of the Swahili language in Egypt. Today, the North African country considers Swahili language to be one of the most important languages in Africa; which is used as a lingua franca even by fellow Nile River countries. There is a relatively long history of Swahili language teaching; beginning in 1967 with the establishment of the Department of African Languages, within the Faculty of Languages and Translation at the Al-Azhar University. Since then, many students have learned Swahili and become either Swahili teachers; editors in Egyptian Radio for East African countries; or Swahili language translators at Al-Azhar centres. The establishment of other departments at three other universities - namely, Ain Shams University, Cairo University, and most recently Aswan University - has helped to grow and develop Swahili language teaching. Egypt continues to take steps to advance the teaching and use of Swahili language with the aim of strengthening relations between it and several East and Central African countries, where it remains the main language of communication.

Utangulizi

Kiswahili kimepewa shime kubwa barani Afrika kwa kuwa ndiyo lugha yenye umuhimu mkubwa kabisa kuhakikisha mawasiliano baina ya Waafrika wapatao milioni 100. Lugha ya Kiswahili imekuwa ni lugha rasmi na ya msingi katika mashirika, vyuo, taasisi na vyombo vya habari katika nchi kadhaa barani Afrika na ulimwengu mzima. Kwa kuwa Kiswahili kimekuwa ni lugha ya mawasiliano na shughuli mbali mbali barani humo, imekuwa ikifundishwa katika nchi kadhaa ikiwemo Misri. Kwa kweli kufundisha Kiswahili hakukutokea ghafla, bali ilikuwa ni miongoni mwa hatua nyingi zilizochukuliwa kwa lengo la kuimarisha mahusiano baina ya Misri na nchi za Afrika Mashariki.

Kwa hakika kufundisha na kutumia lugha ya Kiswahili, kumekua sana katika miaka ya hivi karibuni, ambapo wanafunzi wanaosoma na kuishughulikia lugha hiyo wamekuwa wengi na wanaongezeka kwa kasi. Kiswahili hakipo katika vyuo vikuu na taasisi za elimu tu, bali pia kipo katika mashirika, Idara mbali mbali za kiserikali na za kibinafsi. Sera ya Misri ya kuimarisha mahusiano na nchi za Kiafrika imewajibisha kuzingatia sana Kiswahili kwani ni lugha inayotumika zaidi katika mawasiliano katika nchi kadhaa barani Afrika. Katika makala hii mtafiti anaonesha hali ya Kiswahili ilivyo nchini Misri katika nyanja mbali mbali za maisha kama vile elimu, vyombo vya habari, siasa na uchumi, ufasiri na utamaduni, ulinganiaji na masuala ya kidini, historia na ustaarabu.

Ufundishaji wa Kiswahili nchini Misri

Kwa ujumla, Kiswahili kilipata umaarufu mkubwa nchini Misri kama lugha mashuhuri zaidi miongoni mwa lugha za Kiafrika ambazo zinafundishwa nchini humo. Kiswahili kina nafasi kubwa katika uwanja wa elimu na masomo yanayohusiana na ufundishaji wa lugha za kigeni nchini Misri. Inatosha kufahamu kwamba vyuo vikuu vya kimisri vinasomesha lugha hiyo tangu mnamo miaka hamsini na kuwa maktaba za vyuo vikuu hivyo vina machapisho mengi yanayohusiana na lugha hiyo zikiwemo tafiti, tasnifu, makala na kazi nyingi zinazohusiana na lugha hiyo.

Kufundisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Al-Azhar

Kwa hakika kufundisha Kiswahili nchini Misri kumeanza kabla ya miaka hamsini takriban, kupitia kuanzishwa Idara ya Lugha za Kiafrika katika Kitivo cha Lugha na Ukalimani, Chuo Kikuu cha Al-Azhar¹. Kwa kuwa Al-Azhar Al-Shareif inashughulikia sana ufundishaji wa sheria ya kiislamu na kuwaandaa maimamu kwa waislamu wa nchi mbali mbali duniani, Taasisi hiyo yenye historia ndefu imeanzisha Idara ya Lugha za Kiafrika kwenye Chuo Kikuu cha Kiislamu kiitwacho Chuo Kikuu cha Al-Azhar. Idara hiyo iliyofunguliwa mwaka 1967 na ilikuwa na lengo la kutoa mafunzo yanayohusiana na historia, ustaarabu, utamaduni, fasihi na lugha. Wakati wa kuanzisha Idara hiyo, Misri ilikuwa ikitambua sana mchango muhimu wa kuwasiliana na nchi za Kiafrika hasa zile nchi ambazo zina mahusiano ya kihistoria na nchi hiyo ya Afrika Kaskazini. Idara ya Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Al-Azhar mwanzoni kilichagua lugha mbili; Kizulu na Kiswahili na kuzifanya ni lugha za mwanzo kabisa kufundishwa katika idara hiyo.

Lengo kuu la kuanzisha idara ya kufundisha lugha za Kiafrika ni kuwapa wahitimu wa Al-Azhar masomo yanayowawezesha kuwa wahitimu wanaoweza kuwasiliana na watu kwa lugha zao na kuwa na uelewa kuhusu tamaduni na historia yao. Malengo mengine ni kuimarisha mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi baina ya Misri na nchi za Kiafrika na kuendeleza mahusiano ya kihistoria baina ya Misri na nchi hizo. Na kwa ajili ya kutekeleza ujumbe wa Al-Azhar Al-Shareif wa kuwapa Waislamu wa nchi mbali mbali duniani elimu ya kisheria, Idara ya Masomo ya Kiislamu kwa Lugha za Kigeni ilianzishwa, lugha ya Kiswahili ikawa ni lugha ya kiafrika ya pekee inayosomesha katika idara hiyo. Tangu mwaka 1967 mpaka sasa, Idara ya Lugha za Kiafrika imesomesha Kiswahili kama ni lugha ya kwanza ya Kiafrika ikifuatiwa na lugha nyingine kama vile; Kihansa, Kifulani na Kiamhari.

Jambo la kufurahisha ni kwamba wahitimu wengi wa idara hiyo waliofundishwa Kiswahili wameweza kupata nafasi za kazi zinazohusiana na Kiswahili. Kazi hizo ni kama vile kuwa walimu, watafiti wa Kiswahili, wafasiri katika mashirika ya vyombo vya habari au washauri katika masuala ya kiafrika katika wizara tofauti nchini Misri. Idara ya Lugha za Kiafrika inaendeshwa na wamisri

¹ Wakati ule ilikuwa Taasisi ya Lugha na Ukalimani kisha ikageuzwa kuwa Kitivo cha Lugha na Ukalimani.

HALI YA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI MISRI

na Waswahili wenzao bega kwa bega kwa ajili ya kutekeleza malengo na makusudio ya kuanzisha idara hiyo. Katika Idara ya Lugha za Kiafrika, mwanafunzi hupata mafunzo yake kwa muda wa miaka minne kwa lugha ya Kiswahili, ambapo anasoma masomo ya kifasihi na kilughawiya (Isimu).

Lugha ya Kiswahili imezingatiwa sana katika shughuli mbali mbali zinazohusiana na lugha hiyo nchini Misri kama vile; tafsiri za kazi kadhaa kutoka Kiswahili kwenda Kiarabu na kutoka Kiarabu kwenda Kiswahili, kutoa makala, tafiti na tasnifu kuhusu lugha hiyo, kuanza hatua za kupitisha ushirikiano baina ya Wamisri na wenzao Waswahili katika mambo yanayohusiana na lugha, utamaduni, ufundishaji n.k. Kwa hivyo, kufundisha Kiswahili ikawa hatua ya mwanzo kabisa miongoni mwa hatua nyinginezo nyingi za kuimarisha mahusiano baina ya Misri na Afrika Mashariki.

Kufundisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kairo

Kutokana na umuhimu wa lugha hiyo, Chuo Kikuu cha Kairo ambacho ni kikubwa zaidi nchini Misri kilianzisha Chuo cha Tafiti na Masomo ya Kiafrika, ambacho kinashughulikia sana masuala ya kiafrika katika taaluma mbali mbali zikiwemo; historia, siasa, uchumi, jiografia, madini na nyanja nyinginezo. Mnamo mwaka 1970 Rais wa Misri wakati ule, Gamal Abdel-Nasser, alitoa agizo la kuendeleza Chuo cha Tafiti na Masomo ya Kiafrika kwa kuongeza idara ya kusomesha lugha za Kiafrika. Lugha ya Kiswahili na Kihausa ndizo lugha za mwanzo kabisa kusomesha katika idara hiyo. Wengi wa wanafunzi waliojiunga na idara hiyo wakawa wahadhiri wa baadaye wakifundisha yale waliyoyasoma idarani hapo kuhusu lugha, fasihi na utamaduni wa Afrika na hasa Afrika Mashariki ambapo lugha ya Kiswahili inazungumzwa; na Afrika Magharibi ambapo Kihausa kinatumika sana. Inakumbukwa kuwa kipindi cha miaka ya sitini na kendelea, mahusiano kati ya Misri na nchi kadhaa za Kiafrika ikiwemo Tanzania yaliimarika sana na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika harakati za ukombozi wa nchi za Kiafrika. Katika kipindi hicho, wanasiasa wa Kiafrika walikutana nchini Misri kujadili juhudi za kupata uhuru na baadaye kuunda jumuiya inayojulikana kama Umoja wa Afrika. Miongoni mwa wanasiasa maarufu waliokuwa wakihudhuria mikutano hiyo ni Baba wa Taifa Julius Nyerere, rais wa kwanza wa Tanzania baada ya uhuru.

Japokuwa Idara ya Lugha za Kiafrika katika Chuo cha Tafiti na Masomo ya Kiafrika imeongeza lugha nyingine hadi zikawa lugha saba (ambazo ni pamoja na Kiswahili, Kihausa, Kiamhari, Kiluganda, Kifulani, Kimandingo na Kisomali), Kiswahili ndiyo lugha ya msingi kabisa ambapo mwanafunzi inambidi kusoma ama Kiswahili au Kihausa au Kiamhari katika kiwango cha kwanza kama lugha ya msingi na anaweza kuchagua lugha moja kutoka katika lugha nyinginezo kama lugha ya pili.

ALAA SALAH

Kufundisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Ain Shams

Haukupita muda mrefu baada ya kuanzishwa Idara ya kusomesha lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Al-Azhar na Chuo Kikuu cha Kairo, Idara ya Lugha za Kiafrika ilianzishwa katika Chuo Kikuu cha Ain Shams kwenye Kitivo cha Lugha. Idara hiyo iliyoanza kazi yake miaka ya 1980, ilianza kusomesha lugha mbili kuu za kiafrika; Kiswahili na Kihausa. Baada ya miaka michache, idara hiyo ilisimamishwa kazi zake, lakini ilifunguliwa tena mwaka 2011 na kuwa mojawapo ya idara kuu za Kitivo cha Lugha ikizingatia sana kusomesha lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wake kama ni lugha ya msingi na kwa wanafunzi wa idara nyinginezo kama ni lugha ya pili.

Hata hivyo, licha ya kuwa miaka kadhaa imepita tangu kufunguliwa upya Idara hii ya Lugha za Kiafrika katika Kitivo cha Lugha cha Chuo Kikuu cha Ain Shams na wanafunzi kujiunga tena na idara hiyo wakiwa na hamu kubwa sana ya kujifunza lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya msingi katika idara hiyo, bado wahitimu wa idara hiyo ni wachache, lakini bila shaka wana nafasi kubwa ya kuwa watafiti wa mwanzo wa lugha ya Kiswahili na fasihi yake chuoni humo.

Idara ya Lugha za Kiafrika inalenga kuimarisha masomo yanayohusiana na lugha ya Kiswahili kwa kuwapa wanafunzi wake nafasi ya kupata masomo ya juu na maandalizi ya kupata shahada ya uzamili na uzamivu pamoja na kupata mazoezi zaidi yanayotarajiwa kuwarahisishia wanafunzi na wahitimu hao kuwasiliana na Waswahili kwa urahisi na kuwa na kuwa na uwezo wa kutumia lugha hiyo kwa ufasaha.

Kufundisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Aswan

Kama kilivyo Chuo cha Tafiti na Masomo ya Kiafrika cha Chuo Kikuu cha Kairo, Chuo Kikuu cha Aswan, kilichopo kusini mwa Misri, pia kilianzisha Taasisi ya Tafiti na Masomo ya Kiafrika na Mambo ya Nchi za Bonde la Mto Nile. Taasisi hiyo inajumuisha vitengo mbali mbali kikiwemo Kitengo cha Lugha za Kiafrika ambacho pamoja na lugha nyingine, kinasomesha pia Lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa taasisi hiyo ni wale waliokwisha hitimu shahada ya kwanza katika kitivo chochote na wakataka kupata diploma mahususi katika mambo ya Kiafrika. Jambo la kuzingatiwa ni kuwa taasisi hiyo japokuwa ilianzishwa hivi karibuni, lakini wanafunzi waliojiunga nayo sio wachache.

Kiswahili katika Uwanja wa Masomo

Kutokana na maelezo yaliyopita hapo juu, inabainika kuwa ufundishaji wa Kiswahili nchini Misri una historia ndefu na kwamba Kiswahili kimepata hadhi kubwa hadi kushika nafasi ya kwanza miongoni mwa lugha nyingine za Kiafrika kwa upande wa ufundishaji wa lugha nchini humo. Pia, Kiswahili kinasomwa sana na kinapewa nafasi kubwa sana na wahusika wa elimu wa Misri ambao wanaendelea kufanya juhudi mbali mbali kwa ajili ya kuboresha hali ya ufundishaji wa lugha hiyo.

HALI YA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI MISRI

Vile vile, nafasi ya Kiswahili katika uwanja wa ufundishaji nchini Misri inathibitisha namna nchi hiyo inavyozingatia lugha ambayo ndiyo lugha yenye asilimia 60 au zaidi ya wazungumzaji wake ambao mataifa yao yanashirikiana na Misri katika mto wa Nile ambao ndio mshipa wa uhai wa nchi hiyo na nchi mbali mbali za Mashariki na Kati ya barani Afrika.

Kufundisha Kiswahili kwenye vyuo vikuu, taasisi za masomo ya juu na vyuo vya kibinafsi, huwa ni kielelezo cha kiwango cha umuhimu wa lugha hii na kwamba viongozi wa nchi hiyo wanatambua sana umuhimu wa lugha hii wa kuziunganisha nchi mbali mbali za Kiafrika, hasa ikijulikana kwamba Kiswahili na Kiarabu ndizo lugha zilizoenea zaidi barani Afrika. Inakumbukwa kwamba kazi ya kufundisha Kiswahili nchini Misri inatekelezwa kwa kushirikiana baina ya walimu Wamisri waliopata masomo ya kujifunza lugha hiyo na baadhi ya Waswahili wanaoishi nchini Misri. Walimu wa Kiswahili nchini Misri wanajitahidi sana kupata uzoefu na ujuzi wa kutosha ili waweze kwenda sambamba na mbinu, nadharia, istilahi na maendeleo ya kisasa ya lugha hiyo. Kwa hiyo, mikataba ya ushirikiano baina ya pande mbili; Misri na nchi za Afrika Mashariki katika uwanja wa ufundishaji wa Kiswahili ilihitajika sana. Jambo lililotekelezwa kwa kufunga mkataba wa ushirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Al-Azhar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa ajili ya kubadilishana mawazo na kuendeleza hali ya ufundishaji Kiswahili na kuimarisha mahusiano ya kimafundisho na kimafunzo baina ya pande mbili.

Nyanja za Matumizi ya Kiswahili nchini Misri

Kwa hakika matumizi ya Kiswahili nchini Misri hayakuwa katika uwanja wa kuifundisha lugha hiyo tu, bali nchi hiyo inatumia Kiswahili katika nyanja nyingine mbali mbali kama vile; habari, shughuli za kisiasa na uchumi, mambo ya kitamaduni, masuala ya dini na shughuli za ufasiri na tarjuma. Katika mistari ifuatayo mtafiti wa waraka huu anazungumzia matumizi ya Kiswahili katika nyanja mbali mbali nchini Misri.

Kiswahili katika Uwanja wa Vyombo vya Habari

Idhaa ya Kimisri kwa Kiswahili

Inafahamika kuwa vyombo vya habari ni njia muhimu sana katika mawasiliano ya zama hizi, na kwamba vyombo hivyo vinaathiri sana kuunda uelewa wa mataifa na mitazamo yake. Bara la Afrika lilikuwa na haja kubwa sana ya kuunganishwa hasa katika kipindi cha baada ya kupata uhuru kutokana na ukoloni, ambapo nchi kadhaa zilikuwa zinaanza hatua za mwanzo kabisa za kuunda jamii mpya na kujenga nguzo za dola na utawala wa baada ya uhuru. Kubadilishana mawazo, tajiriba, maelezo na kuimarisha mawasiliano yao, yote haya yalikuwa ni malengo makuu ya kuanzisha Idhaa ya Kimisri inayosikika nchi mbali mbali barani Afrika. Raisi wa Misri wa wakati huo, Gamal Abdul-Nasser ndiye aliyeanzisha Idhaa ya Kimisri kwa lugha za kigeni.

ALAA SALAH

Kitengo cha Idhaa ya Kiswahili kilipewa umuhimu na uangalifu mkubwa zaidi kuliko vitengo vingine. Kuanzia mwaka 1970, Idhaa ya Kimisri imekuwa inarusha vipindi vingi kwa lugha mbali mbali za kiafrika. Hata hivyo, kipindi cha Kiswahili ndicho kipindi cha kale zaidi kuliko vipindi vingine vingi. Waswahili wengi wamewahi kufanya kazi katika kipindi hicho wakiambatana na wenzao Wamisri waliojifunza Kiswahili.

Shirika la Taifa la Maelezo

Ikiwa idhaa inashughulikia kufuatilia habari zinazohusiana na mambo ya kimisri na kiafrika kwa ujumla, ikiwatangazia Waafrika na wasikilizaji lengwa kwa lugha zao, Shirika la Taifa la Maelezo linashughulikia kufuatilia habari za Misri na ulimwenguni kote na hasa kutambua, kuonesha na kueleza hali ya mambo ilivyo nchini Misri. Shirika hilo lililoanzishwa hapo mwaka 1954 lina Idara mbali mbali zinazoshughulikia utoaji taarifa na machapisho yanayodhamiria kutoa fikra kuhusiana na Misri na harakati zake ndani na nje ya nchi hiyo. Pia, shirika linazingatia kuwasiliana na nchi mbali mbali duniani na kubadilishana mawazo kuhusu masuala ya pamoja. Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha za msingi katika sehemu ya mambo ya kiafrika kwenye shirika hilo. Wahusika wa sehemu ya mambo ya kiafrika katika Shirika hilo wanafuatilia sana taarifa zinazotolewa katika nchi za kiafrika zikiwemo nchi za Afrika Mashariki ambapo lugha ya Kiswahili ndiyo inayotawala mawasiliano na vyombo vya habari. Shirika la Taifa la Maelezo linatoa matoleo mengi kama vile ripoti, taarifa, vitabu na jarida la kitaaluma. Matoleo haya japokuwa yapo kwa lugha ya Kiarabu yanahusiana na masuala yote yanayofungamana na hali ya mambo nchini Misri, barani Afrika na ulimwenguni kote.

Kiswahili katika Shughuli za Kisiasa na Kiuchumi

Kwa kuwa Misri ni nchi iliyopo kaskazini mwa Afrika ambapo ni mwisho wa mto Nile, nchi hiyo inazingatia sana kuendeleza mahusiano makubwa na ya kihistoria na nchi mbali mbali za kiafrika. Nchi za Bonde la Mto Nile ambazo ni nchi za Mashariki na Kati mwa Afrika zina mfungamano na mahusiano makubwa ya kihistoria, kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Lugha mbili kuu za mahusiano na mawasiliano haya ni Kiarabu na Kiswahili. Hata hivyo lugha ya Kiingereza inatumika katika baadhi ya mawasiliano baina ya Misri kwa upande mmoja na Nchi hizo za kiafrika kwa upande mwingine. Hata hivyo, Kiswahili na Kiarabu hazikukosa nafasi zao katika shughuli mbali mbali za pamoja baina ya nchi hizo. Nchini Misri; wanafunzi, watafiti na wataalamu wengi wanaoshughulikia mambo yanayohusiana na ushirikiano baina ya nchi hiyo na nchi nyingine katika nyanja mbali mbali, hawana budi kufahamu lugha kuu inayozungumzwa zaidi barani Afrika ikiwemo Kiswahili. Katika Idara ya Sayansi za Kisiasa na Shughuli za Kiuchumi, wanafunzi wanatakiwa kutambua historia na maendeleo ya nchi husika ambazo zina mahusiano na Misri.

HALI YA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI MISRI

Vile vile, Misri imechangia sana kuzisaidia nchi mbali mbali za Kiafrika kupata uhuru wake. Isitoshe, baada ya kupata uhuru, nchi kadhaa zinaendelea mafungamano yao na Misri kupitia mahusiano yenye kulenga kubadilishana mawazo na mashauriano kuhusu mbinu za kuimarisha na kugundua mifumo mipya ya utawala na mbinu za kujenga jamii ya baada ya uhuru. Kwa kweli historia inaonesha kuwa nchi za kiafrika hazitopata maendeleo wala utulivu bila ya kushirikiana pamoja na kubadilishana mawazo na ujuzi wa kuendesha mambo yao bila ya kutegemea sehemu fulani. Waafrika walipojitegemea wakijitahidi kujikomboa, kujiendeleza na kuzitetea nchi zao na utamaduni wao walifaulu wakawashinda maadui zao ambao sio tu wanataka kuzikalia nchi zao na kuzipora utajiri wao, bali maadui hao pia wanataka kuwasambaratisha, kuwazozanisha, kupotezea utambulisho wao wa kiafrika, kuwakosesha utamaduni wao ikiwemo kuachana na Lugha zao.

Kiswahili na Kukuza Utamaduni wa Kiafrika

Kwa kuwa lugha ni nguzo ya utamaduni ambayo inatoa picha kamili ya utamaduni wowote, na kuyawezesha mataifa yajielezee na kufafanua hali yao ya kisasa na ya zamani, lugha imekuwa ndiyo chombo cha msingi cha mawasiliano, na ni kipengele kisichowezezana kutengwa katika shughuli za kitamaduni na kistaarabu. Utamaduni na Ustaarabu wa Kiafrika ulielezwa ulimwenguni kote kupitia lugha mbali mbali za kijadi na za kisasa. Kiswahili kinabeba dhima na jukumu la kuelezea utamaduni wa nchi za Afrika Mashariki na baadhi ya maeneo ya Afrika ya Kati. Fasihi ya Kiswahili (simulizi na andishi) ilienea sana duniani kote, ikielezea pande mbali mbali za maisha ya Waswahili na namna walivyohusiana wenyewe kwa wenyewe na walivyowasiliana na mataifa mengine.

Inajulikana sana kuwa fasihi, urithi, ada, mila na desturi, mabaki ya kale (majengo, misikiti, majumba n.k.) ndizo nguzo za utamaduni wa umma wowote. Haya yote yanaelezwa kupitia lugha ambayo inatumiwa kutoa maelezo na taarifa za kutosha kuhusu utamaduni. Mashairi, hadithi, riwaya na makala za Kiswahili vinatumika kwa lengo la kutambua utamaduni na historia ya jamii ya Kiswahili. Kama tulivyobainisha hapo juu, vyo vya kufundisha Kiswahili nchini Misri vinatoa mafunzo ya kilughawiya na kifasihi kwa kutegemea machapisho mengi ya Kiswahili yaliyotolewa nchi mbali mbali duniani. Kwa ufupi, lugha ya Kiswahili ndiyo chombo cha kueleza utamaduni na ustaarabu wa maeneo ya Afrika Mashariki. Na katika harakati za kuendeleza na kukuza utamaduni wa Kiafrika na, hasa Mashariki mwa bara hili, Kiswahili kimetumika sana kwa ajili ya kufikia lengo hilo.

Kiswahili na Shughuli za Ulinganiaji na Masuala ya Kidini

Misri ndiyo nchi yenye Al-Azhar Al-Shareif ambayo ni Taasisi ya kiislamu iliyo ya kale zaidi duniani na yenye historia inayozidi miaka elfu moja. Kuwepo kwa Al-Azhar Al-Shareif nchini humo kumeifanya Misri iwe ni kusudio la wanafunzi wanaotoka mataifa mbali mbali ulimwenguni

ALAA SALAH

wakiwa na matarajio ya kupata elimu za kisheria iliyo katika mfumo wa wastani wa Uislamu. Kwa hiyo, taasisi hiyo imekuwa inawapatia maelfu ya wanafunzi hao mafunzo yanayotakiwa kuwasaidia wawe na ujuzi na maarifa ya elimu za kisheria na lugha ya Kiarabu kwa kutaraji kuwa maimamu, walimu walinganiaji watakaporudi makwao. Kwa kweli, wengi wa wanafunzi wageni wanaosoma katika Al-Azhar Al-Shareif ni Waafrika. Kwa hivyo, Al-Azhar imekuwa inazingatia sana kuwapa wanafunzi hawa maandalizi ya kutosha katika masuala mbali mbali. Kwa hakika muamala wa Al-Azhar kwa mambo yanayohusiana na Afrika umekuwa unategemea sana lugha ya Kiswahili, jambo linalobainika kupitia hatua zifuatazo:

- Kuanzisha Idara ya Masomo ya Kiislamu kwa lugha ya Kiswahili, Kitivo cha Lugha na Ukalimani, Chuo Kikuu cha Al-Azhar.
- Kupeleka walimu wa masomo ya kisheria na lugha ya Kiarabu katika nchi za Kiafrika zikiwemo nchi za Afrika Mashariki ambapo Kiswahili kinazungumzwa.
- Kuanzisha Kundi la Kimataifa la Wahitimu wa Al-Azhar waliotoka nchi tafauti duniani, kwa ajili ya kuwasiliana nao na kuwaandalia programu zinazohusiana na mbinu za ulinganiaji na namna ya kuendeleza hotuba za kidini kwa mujibu wa hali halisi ya mambo katika jamii zao.
- Kusimamia ufasiri wa Tafsiri ya Muntakhab ya Qurani Takatifu kwa Kiswahili chini ya anuani: Tafsiri ya *Tafsiri ya Al-Muntakhab* (The Highest Islamic Council 2016).
- Kufasiri baadhi ya vitabu vinavyohusiana na masuala ya kidini kutoka Kiarabu kwenda Kiswahili kama vile *Mimi Ni Mwislamu* (Salah 2010), *Maelezo kwa Mahujaji na Wafanyao Umrah* na vinginevyo (Al-Othaimiin, Abdul-Aziz, Abdul-Muhsin Al-Badr 2016).
- Kufasiri fungu la vitabu la *Al-Fatawa Al-Mua'ssalah*² kwa kushirikiana na Idara kuu ya Fatwa ya Kimisri kwa Kiswahili kwa lengo la kuwafahamisha Waswahili majibu ya maswali mbali mbali ya kifiqhi kwa lugha yao.
- Kuanzisha Kituo cha Al-Azhar cha Kupambana na Fikra Kali kwa lugha za Kigeni na kuichagua lugha ya Kiswahili iwe ndiyo lugha ya msingi ya Kitengo cha lugha za Kiafrika kwenye kituo hicho.³
- Kuanzisha Kituo cha Al-Azhar cha Ufasiri, ambacho kinashughulikia kutoa machapisho muhimu ya kidini kwa lugha mbali mbali na kukichagua Kiswahili kiwe ndiyo lugha inayotumika miongoni mwa lugha za Kiafrika kwenye kituo hicho.

² دار الإفتاء المصرية (2019)، موسوعة الفتاوى المؤصلة، الطبعة الثانية، القاهرة، مصر

Kwa maelezo zaidi unaweza kuangalia kiungo cha Idara Kuu ya Fatwa nchini Misri: <http://www.dar-alifta.org/Foreign/default.aspx?LangID=11&Home=1> <http://www.azhar.eg/observer/> (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 19-04-2023).

³ Mwandalizi wa Makala haya alikuwa msimamizi wa Kitengo hicho, ikumbukwe kuwa Kituo hicho kilichapisha kitabu kwa Kiswahili na makala kadhaa ambazo zinalenga kuwafahamisha vijana waswahili na wengineo kuhusu madhara ya fikra hizo. Kwa maelezo zaidi: <http://www.azhar.eg/observer/> (mara ya mwisho kutembelewa tarehe 22-04-2023).

HALI YA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI MISRI

- Kuwachagua wahitimu wa Idara ya Masomo ya Kiislamu kwa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Al-Azhar, wafanye kazi katika Halmashauri ya Tafiti za Kiislamu inayosimamia masuala ya kuwasiliana na waislamu wa nchi mbali mbali duniani na kushughulikia mambo na masuala yao.
- Kuanza kuandaa Tafsiri mpya ya Maana za Qurani Takatifu kwa Kiswahili ambayo inatarajiwa kutolewa hivi karibuni na wataalamu wa lugha ya Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar.

Kutokana na yaliyopita hapo juu, tunaona kuwa Kiswahili kimekuwa ndiyo lugha inayoshughulikiwa sana na Al-Azhar katika shughuli zake zinazofungamana na masuala ya dini na ulinganiaji. Isitoshe, Wizara ya Waqfu ya Misri inakizingatia Kiswahili kuwa ni lugha mojawapo kuu inayotumika katika shughuli zake kama vile vitabu, makala, hotuba za Ijumaa, n.k. Kwa kutaraji kuwanufaisha Waislamu kutoka nchi tofauti ulimwenguni, Wizara ya Waqfu nchini Misri ilianzisha tovuti yake kwa lugha mbali mbali ikiwemo Kiswahili.⁴

Wataalamu, watafiti, wasomi na wanafunzi wanaotoka maeneo ya Afrika Mashariki wanachangia sana kuimarisha shughuli za kidini kwa lugha ya Kiswahili katika kazi mbali mbali. Kwa hiyo, Mamufti, wahusika na wataalamu wa mambo ya kidini Afrika Mashariki huwa wanaalikwa kuhudhuria mikutano, makongamano na warsha za kazi hizo nchini Misri.

Kiswahili na Shughuli za Tafsiri

Kwa hakika ufasiri ni mojawapo ya njia muhimu za kuimarisha mawasiliano baina ya mataifa mbali mbali, na kuleta ufahamu kuhusu ustaarabu, utamaduni na maisha kwa jumla. Inajulikana kuwa ufasiri ni kuhamisha mawazo fulani kutoka lugha moja kwenda nyingine. Tunaweza kusema kwamba tarjuma ndio daraja ya mawasiliano baina ya mataifa. Kwa maana hiyo, tunasisitiza kuwa yeyote anayetaka kutambua taifa lolote kwa upande wa utamaduni wao, historia yao, mila na desturi zao na maisha yao kwa ujumla, anatakiwa kusoma fasihi yao. Ama akiwa haifahamu lugha yao inambidi apate msaada kwa kusoma tafsiri ya kazi za fasihi yao au urithi wao. Bila shaka, makala haya hayashughulikii historia ya tafsiri baina ya Kiswahili na Kiarabu⁵, bali itatosha kuashiria umuhimu wa tafsiri na tarjuma katika kukuza lugha na kuimarisha mawasiliano baina ya mataifa tafauti.

Kazi zilizotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiarabu na kutoka Kiarabu kwenda Kiswahili ziko nyingi: mashairi, hadithi fupi, riwaya na hata makala kadhaa zilitafsiriwa kutoka Kiarabu kwenda Kiswahili kama vile *Hekaya za Abunuwas* na hadithi za *Alfu-Lela-Ulela*, tafsiri ya kitabu cha Taha Hussein *Ahadi ya Haki* iliyotafsiriwa na Muhammad Suleiman Muhammad na tafsiri ya riwaya ya Naguib Mahfouz *Al-Tariiq* iliyotafsiriwa na Deogratias M. Simba katika kitabu

⁴ Tovuti ya Wizara ya Waqfu ya Misri kwa Kiswahili: <https://web.facebook.com/Wizara-ya-Wakfu-ya-Misri-1110427415643386/> (mara ya mwisho kufunguliwa 19-04-2023).

⁵ Kwa maelezo zaidi kuhusu Tafsiri kati ya Kiarabu na Kiswahili unaweza kurejelea Salah 2018.

ALAA SALAH

kiitwacho *Msako*. Kituo cha Taifa cha Ufasiri nchini Misri kimechapisha kazi nyingi zilizotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiarabu kama vile:

- Riwaya ya *Almasi za Bandia* na Chachage, iliyotafsiriwa na Profesa Abdulhay A. M. Salem, Kituo cha Taifa cha Ufasiri, Misri 2005.
- Hadithi za watoto za *Hadithi Njoo* na Ahmad Ndal, zilizotafsiriwa na Profesa Abdulhay A. M. Salem, Kituo cha Taifa cha Ufasiri, Misri 2005.
- Riwaya ya *Haini* na Adam Shafi, iliyotafsiriwa na Profesa Mohammed I. Abouegl na Bw. Abdullah Muawiyah, Kituo cha Taifa cha Ufasiri, Misri 2010.
- Tamthilia ya *Wakati Ukuta* na Ebrahim Hussein, iliyotafsiriwa na Profesa Mohammed I. Abouegl, Kituo cha Taifa cha Ufasiri, Misri 2010.
- Tamthilia ya *Kilio cha Haki* na Alamin Mazrui, iliyotafsiriwa na Profesa Mohammed I. Abouegl, Kituo cha Taifa cha Ufasiri, Misri 2010.
- Riwaya ya *Vuta N'kuvute* na Shafi Adam Shafi, iliyotafsiriwa na Profesa Mohammed I. Abouegl na Bw. Abdullah Muawiyah, Kituo cha Taifa cha Ufasiri, Misri 2015.
- Kitabu cha *Historia ya Kiswahili* na Shihabuddin Sirajuddin, kilichotafsiriwa na Profesa Abdulhay A. M. Salem, Kituo cha Taifa cha Ufasiri, Misri 2015.

Pamoja na hayo, wataalamu wa Kiswahili wamefanya juhudi kubwa za kutoa kamusi kadhaa za Kiswahili–Kiarabu na Kiarabu–Kiswahili, kuanzia mwaka 1987 ambapo kamusi dogo la Kiswahili–Kiarabu / Kiarabu–Kiswahili lilitolewa na Profesa Mostafa El-Halougi, kisha Kamusi la Al-Wageez (Kamusi Fupi) Kiarabu–Kiswahili na Profesa Abdulhady H. Marzouk, na mwishoni Kamusi la Al-Shaamil Kiswahili–Kiarabu na Kamusi la Al-Shaamil Kiarabu–Kiswahili na Profesa Ali A. Ahmed Shaaban na Profesa Abdulhay A. M. Salem.⁶

Isitoshe, Idara kuu ya kutoa Fatwa nchini Misri ilianzisha mradi wa kufasiri vitabu kadha wa kadha za fatwa, yaani sheria za kiislamu. Mradi huu ulijumuisha lugha nyingi ikiwemo Kiswahili kupitia kufasiri kundi la vitabu viitwavyo: *Al-Fatawa Al-Mua'assala*, ambapo jopo la wataalamu wa lugha ya Kiswahili wanafasiri kundi hilo la vitabu katika kazi inayoendelea mpaka leo.⁷

Aidha Kiswahili kinashughulikiwa sana katika uwanja wa ufasiri katika mahafali za kimatifa kwa ujumla na kiafrika hususan, miongoni mwa mikutano hiyo Mkutano wa Kimataifa wa Al-Azhar wa Kupambana na Ugaidi na fikra kali uliofanyika mwaka 2014, ambapo makala na tafiti za mkutano huo zilitafsiriwa kwa lugha mbali mbali ikiwemo Kiswahili.⁸ Pia, miongoni mwa

⁶ Maprofesa wote waliotajwa ni walimu wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar waliopata Shahada zao za Uzamivu kutoka Vyuo Vikuu mashuhuri nchini Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Misri.

⁷ Miongoni mwa wataalamu wanaoshughulikia kazi hii; Maprofesa; Abdulhay A. M. Salem, Wael N. Ibrahim, Sameh Anwer Ibrahim, Mohammed Tolba Ebeid.

⁸ الأزهري الشريف، الأزهري في مواجهة الفكر الإرهابي، من أعمال مؤتمر الأزهر العالمي لمواجهة التطرف والإرهاب، ترجمة: Yussuf Mwalim Omar (2014)، الأزهري الشريف ومجلس حكماء المسلمين

“Semina ya Kimataifa ya Al-Azhar kwa ajili ya Kukabiliana na Itikadi kali na Ugaidi.”

HALI YA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI MISRI

vitabu vilivyoenea sana ni kitabu cha *Sira ya Mtume katika Dakika Chache*.⁹ Kwa jumla, wahadhiri, watafiti na wanafunzi wa Kiswahili nchini Misri wanafanya juhudi kubwa kuendeleza na kuimarisha matumizi ya lugha hiyo na kuifundisha kwa wengine wengi kwa kuwa wametambua vyema umuhimu wa lugha hiyo kwa kuhudumia nchi yao na kuwasiliana vizuri na nchi za Afrika Masharika na maeneo mengi ya Afrika.

Hitimisho

Katika makala haya mtafiti amejaribu kutoa picha kamili kuhusu hali ya lugha ya Kiswahili nchini Misri kwa pande zote za matumizi yake; ufundishaji, vyombo vya habari, shughuli za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kidini na ufasiri. Pia, mtafiti alidhamiria kudhihirisha namna lugha hii inavyopewa uangalifu nchini Misri kwa kuwa ni mojawapo ya lugha kubwa zaidi barani Afrika na lugha ya maeneo ya Afrika Mashariki ambapo mto wa Nile unapita kabla ya kufika mwisho wake nchini Misri. Mtafiti anaona kuwa mchango wa Kiswahili katika juhudi za kuimarisha mawasiliano baina ya Misri na nchi mbali mbali barani Afrika ni mkubwa na muhimu, jambo linalotubidi sote Waafrika tuzidishie juhudi za kuimarisha mchango wa lugha hiyo na kuzingatia mambo yenye kukuza matumizi yake katika nchi kadhaa barani humu, sio nchini Misri pekee. Pia, mtafiti anaona kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuanzisha Shirika la Wataalamu wa Kiswahili litakalokusanya wataalamu, watafiti na wanafunzi wa lugha hiyo walipo popote duniani.

Aidha, kwetu sisi wadau wa Kiswahili katika nchi mbali mbali tunatakiwa kupanga mikutano na makongamano yanayokutanisha wadau wa Kiswahili duniani wabadilishane mawazo na ujuzi kwa lengo la kuendeleza lugha hiyo kwa mujibu wa hali ya mambo ilivyo. Licha ya hayo, tunatarajia kuanzisha maktaba kuu ya Kiswahili ya kielektronika ili watafiti ambao wapo popote ulimwenguni waweze kupata machapisho, tafiti, makala, taarifa, kamusi na matoleo mbali mbali yahusianayo na Kiswahili bila ya kuwa na haja ya kusafiri huku na kule. Aidha, tumeazimia kuifanya lugha ya Kiswahili iwe ni lugha ya kwanza miongoni mwa lugha za kiafrika na kuifundisha katika Skuli za Sekondari katika nchi mbali mbali za kiafrika ili kuwatayarisha wanafunzi wawe na uelewa japo mdogo unaohusu lugha hiyo yenye nafasi ya kwanza kutimiza malengo ya mawasiliano baina ya waafrika wapatao milioni 200.¹⁰ La mwisho tunasema kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayostahiki kupewa shime na nafasi zaidi kwa maslahi ya waafrika wote sio waswahili tu, basi tujitahidi kufanya hivyo kwa pamoja tukitangaza kuwa wamisri wako tayari kujifunza na kutunza lugha hiyo.

⁹ ناصر الزهراني، السيرة النبوية في دقائق *Sira ya Mtume katika Dakika Chache*، ترجمة: علي أحمد شعبان & وائل نبيل إبراهيم (2016)، دار نشر السلام عليك أيها النبي، مكة المكرمة، المملكة العربية السعودية.

¹⁰Wazungumzaji wa Kiswahili ni zaidi ya milioni 200-Prof. Aldin Mutembei, 7 Mei 2018, katika mazungumzo na tovuti ya Umoja wa Mataifa, kiunganisho: <https://news.un.org/sw/story/2018/05/1014242> (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe19-04-2023).

Marejeleo

Marejeleo ya Kiswahili na ya Kiingereza

Hussein, Taha. n.d. *Ahadi ya haki*, transl. by Muhammad S. Muhammad. Cairo: Baraza Kuu la Uislamu.

Mahfouz, Naguib. 2004. *Msako*, transl. by Deogratias M. Simba. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Salah, Mohammed Ashraf. 2008. *Mimi ni Mwislamu*, transl. by Abdullah Mu'awiya Abdul-Rahman 2010, Al-Khulafaa Al-Rashidiin & Al-Fath Al-Islamy Publishing House, Egypt.

Sh. Mohammed Swaleh Al-Othaimiin, Prof. Sulieman bin Swaleh bin Abdul-Aziz, Dkt. Habib bin Mu'alla na Abdul-Raziq bin Abdul-Muhsin Al-Badr. 2015. *Maelezo kwa Mahujaji na Maelezo kwa wafanyao Umrah*, transl. by Prof. A. Hay Salem na Alaa Salah Abdul-Wahed 2016. Saudi Arabia: Wizara ya Masuala ya Kiislamu na Ulinginaji.

The Highest Islamic Council. 1961. *Tafsiri ya Al-Muntakhab*, transl. by Shaaban, A. Ali, Abouegl, Mohmmmed I., Marzouq, Abdul-Hadi H. na Mua'awiya, Abdullah 2007.

Marejeleo ya Kiarabu

إبراهيم حسين، *حاجز الزمن Wakati Ukuta*، ترجمة: محمد إبراهيم محمد أبو عجل (2010)، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

أحمد ندالو، *هيا نحكي Hadithi Njoo*، ترجمة: عبد الحي أحمد محمد سالم (2005)، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

الأزهر الشريف، *الأزهر في مواجهة الفكر الإرهابي، من أعمال مؤتمر الأزهر العالمي لمواجهة التطرف والإرهاب*، ترجمة: Yussuf Mwalim Omar (2014)، الأزهر الشريف ومجلس حكماء المسلمين

"Semina ya Kimataifa ya Al-Azhar kwa ajili ya Kukabiliana na Itikadi kali na Ugaidi".

تشاتشاجي، *الماس الزائف Almasi za Bandia*، ترجمة: عبد الحي أحمد محمد سالم (2005)، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

الطوجي، مصطفى حسين (1987)، *قاموس بسيط: عربي - سواحيلي، سواحيلي - عربي*، دار البيان، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

دار الإفتاء المصرية (2019)، *موسوعة الفتاوى المؤصلة، الطبعة الثانية، القاهرة، مصر.*

شافي آدم شافي، *الخائن Haini*، ترجمة: محمد إبراهيم محمد، عبد الله معاوية (2010)، سلسلة الإبداع القصصي، العدد 1422، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

شافي آدم شافي، *الشد والجذب Vuta N'kuvute*، ترجمة: محمد إبراهيم محمد أبو عجل، عبد الله معاوية عبد الرحمن (2015)، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

شعبان، علي علي أحمد & سالم، عبد الحي أحمد محمد (2015)، *القاموس الشامل: سواحيلي - عربي*، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

HALI YA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI MISRI

شهاب الدين سراج الدين، *تاريخ اللغة السواحيلية Historia ya Kiswahili*، ترجمة: عبد الحي أحمد محمد سالم (2015)، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

علي مزروعى، *صرخة حق Kilio cha Haki*، ترجمة: محمد إبراهيم محمد أبو عجل (2010)، المركز القومي للترجمة، وزارة الثقافة، القاهرة، جمهورية مصر العربية.

مرزوق، عبد الهادي حامد (2017)، *القاموس الوجيز: عربي-سواحيلي*، محمد علي البرواني.

ناصر الزهراني، *السيرة النبوية في دقائق Sira ya Mtume katika Dakika Chache*، ترجمة: علي علي أحمد شعبان & وائل نبيل إبراهيم (2016)، دار نشر السلام عليك أيها النبي، مكة المكرمة، المملكة العربية السعودية.

Tovuti

Akaunti ya Facebook ya Wizara ya Waqfu ya Misri kwa Kiswahili: <https://web.facebook.com/Wizara-ya-Wakfu-ya-Misri-1110427415643386/> (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 19-04-2023).

Tovuti ya Kituo cha Al-Azhar cha Ufasiri: <http://www.azhar.eg/act/en-us/> (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 19-04-2023).

Tovuti ya Kituo cha Idara kuu ya Fatwa kwa Kiswahili: <http://www.dar-alifta.org/Foreign/default.aspx?LangID=11&Home=1> (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 19-04-2023).